**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

**Kumb.Na.JA.9/259/01/A/109** **14 JUNI, 2022**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Kwa niaba ya Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Wakala wa Chuo ch Taifa cha Utalii (NCT), Katibu wa Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi Wa Umma anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi tano **(5)** kama zilivyoainishwa katika tangazo hili.

### 1.0 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)

Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) ni Taasisi ya Umma ambayo iko chini ya Wizara yenye dhamana ya utamaduni. Baraza liliundwa kwa Sheria ya Bunge Na. 27 ya mwaka 1967 na marekebisho yake. Kutokana na Sheria hii Baraza ndilo Wakala wa Serikali lenye mamlaka ya kusimamia na kuratibu shughuli za wadau wote wanaokuza Kiswahili katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Baraza ni mdau muhimu wa maendeleo ya Kiswahili kimataifa.

### 1.0.1 MCHUNGUZI LUGHA DARAJA LA II (LANGUAGE II) - NAFASI 1

### 1.0.2 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kusoma miswada ya vitabu vya kitaaluma na kushauri kuhusu lugha iliyotumika;
ii. Kutoa mapendekezo ya kuthibitisha lugha katika miswada;
iii. Kusaidia kufuatilia kazi za wanataaluma zinazohitaji kuhaririwa;
iv. Kuchunguza makosa ya matumizi ya lugha katika vyombo vya habari nchini na kuyatolea taarifa kwenye mamlaka husika;
v. Kuandika Makala zinazohusiana na masuala ya lugha ya Kiswahili; na

vi. Kufanya kazi nyingine atakazopewa na mkuu wake wa kazi.

**1.0.2 SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa wenye Shahada ya kwanza katika kozi za Ualimu au Lugha zinazohusisha somo la Kiswahili kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali. Awe na uwezo wa kutumia kompyuta.

**1.0.4 NGAZI YA MSHAHARA**

Kwa kuzingatia Ngazi za mishahara ya **BAKITA PGSS 6**

**1.0.5 MSANIFU LUGHA DARAJA II (LANGUAGE STANDARDIZER II)-NAFASI 1**

**1.0.6 MAJUKUMU YA KAZI**

i. Kusaidia kufanya kazi za utafiti kuhusu istilahi za masomo mbalimbali;
ii. Kukusanya na kuchambua istihali mbalimbali kwa ajili ya usanifishaji;
iii. Kuandaa orodha ya istilahi mbalimbali kwa ajili ya kutayarisha kamusi ndogondogo za taaluma; na
iv. Kufanya kazi nyingine atakazopewa na mkuu wake wa kazi.

**1.0.7 SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa wenye Shahada ya kwanza katika kozi za Ualimu au za Lugha zinazohusisha somo la Kiswahili kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali. Awe na uwezo wa kutumia kompyuta.

**1.0.8 NGAZI YA MSHAHARA**

Kwa kuzingatia viwango vya **BAKITA PGSS 6**

**2.0 CHUO CHA TAIFA CHA UTALII (NCT)**

Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) kilianzishwa kama Wakala wa Serikali chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii tarehe 24 Januari 2003 kwa Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya mwaka1997. Chuo cha Taifa cha Utalii kinahusika katika kutoa Mafunzo, Utafiti na Ushauri katika Sekta ya Ukarimu, Utalii na Uratibu wa matukio.

**2.0.1 MPISHI DARAJA LA II - NAFASI 1**

**2.0.2 KURIPOTI KWA: MENEJA WA BIASHARA**

**2.0.3 KITUO CHA KAZI: NCT KAMPASI YA BUSTANI – DAR ES SALAAM**

**2.0.4 MAJUKUMU YA KAZI**

i. Kufanya usafi wa jiko;

ii. Kupika vyakula vya aina mbalimbali;
iii. Kuhakikisha vyombo vya kupikia vinakuwa safi;
iv. Kutayarisha orodha ya vyakula vya mlo kamili (balanced diet);
v. Kupika vyakula vya kitaalam;
vi. Kuhakikisha chakula kinaandaliwa kwa muda muafaka;
vii. Kuahakikisha usalama wa jiko na chakula; na
viii. Kutekeleza majukumu mengine utakayopangiwa na msimamizi wako

**2.0.5 SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa wenye elimu ya kidato cha Nne (IV) au kidato cha Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/ Cheti (Technician Certificate) katika fani ya Mapishi (Food Production/ Culinary Arts) kutoka Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

**2.0.6 NGAZI YA MSHAHARA**

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali TGS C.

**MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.**

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45 isipokuwa kwa wale tu walioko kazini.
ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
iii. **Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa Waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo.**
iv. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed C.V**) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini **(referees**) watatu wa kuaminika.
v. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vilivyithibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
    - Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificates.
    - Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI

- Computer Certificate
- Vyeti vya kitaaluma (Professional certificates from respective boards)

vi. **Testmonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**

vii. **Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).**

viii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

ix. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na CAC. 45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.

x. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

xi. **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 27 Juni, 2022.**

**Muhimu:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu. anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

***KATIBU***
***OFISI YA RAIS***
***SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA***
***S.L.P. 2320 DODOMA.***

*i.* ***Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo;***

***http://portal.ajira.go.tz/*****(Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sektretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa *'Recruitment Portal'*)**

*ii.* **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.**

Limetolewa na;

**KATIBU**
**SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**